


- Virutubishi kwa mimea ijao kutokana na majani yanayoanguka na nitrojeni iliyoongezwao mchangani.

Kumbuka

Samadi na mbolea ya majani zinapotumiwa pamoja na mbolea ya madini, ongezeko MARADUFU ya mahindi ya kiwango kizuri ndiyo matokeo.



Mazao ya juu ya mahindi



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Kibunja C.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kabete

S.L.P. 14733-00800, Nairobi

Simu: 254-20-4444144

Baruapepe: cdnar1@icconet.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 17 / 2008

Shilingi Ishirini za Kenya

Changanya samadi na mbolea ya madini kwa mavuno ya juu



Utangulizi

Kulima mfululizo bila ya kuongezea rutuba kwa udongo hatimaye husababisha mazao duni.

Virutubishi vilivyo muhimu sana kwa mimea ni fosfarasi na nitrojeni. Hivi hupakina kwenye mbolea za shambani na pia zile za madini.

Mbolea za aina hizi mbili zinapotumiwa kwa pamoja, nafaka za mahindi huongezeka maradufu.

Utunzaji wa rutuba katika mchanga

Kutayarisha shamba

- Tayarisha shamba kabla ya mvua kuanza.
- Tengeneza mitaro, umbali wa sentimita 75 au futi



Shamba lililotayarishwa

- moja na nusu.
- Chimba mashimo ya kina cha sentimita 25 (mbegu moja) au sentimeta 50 (mbegu mbili) kwenye mitaro.

Kupanda

- Weka nusu mkebe wa mbolea iliyokomaa vyema kwa kila shimo wiki mbili kabla ya kupanda.
- Weka mbolea ya fosfarasi (kifuniko cha soda kwa kila shimo) wakati wa kupanda mahindi (changanya vizuri shimoni).
- Panda mbegu zilizopendekezwa katika eneo lako (kwa mfano H 513 katika nyanda za kati na H 614 katika nyanda ya juu nk) kabla ya mvua.
- Funika kwa mbolea ya nitrojeni (kizibo kimoja cha soda cha CAN kwa kila mmea) baada ya majuma manne ya kupanda (inapokuwa na matawi).



Hatua ya kuwa na matawi

- Katika maeneo ya mvua nyingi, tumia mbolea ya CAN mara mbili tofauti ili kuimarisha uwezo wake (baada ya juma la nne na la saba baada ya kupanda).

Kupalilia

- Palilia na udhibiti kwekwe mara kwa mara ili kuzuia mashindano ya virutubishi vilivyoongezewa pamoja na unyevu ulioko.

Kilimo cha mzunguko au pamoja na mimea mseto

- Zungusha kilimo cha mahindi au upande pamoja na mimea jamii ya kunde kama vile maharagwe, dengu nk. Hizi huongeza kiwango cha nitrojeni na faida zingine kwa mahindi kama vile:
 - Kuuvunja mzunguko wa wadudu waharibifu
 - Kutatiza hatua za maisha ya wadudu
 - Matumizi mazuri ya kipindi kati ya misimu miwili.



Ndengu zilizopandwa kwa mpishano na mahindi